



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UZINDUZI WA AWAMU YA PILI YA MRADI WA KULIJENGEA UWEZO BUNGE, (LEGISLATIVE SUPPORT PROJECT II).

Bunge la Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) linautaarifu umma kuwa kesho tarehe 14 Septemba, 2017 kutakuwa na uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Mradi wa kulijengea uwezo Bunge. Hafla ya Uzinduzi huo itafanyika katika Ukumbi wa Bunge kuanzia saa 7:00 mchana na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka Serikalini na Nchi Wafadhili.

Awamu ya Pili ya mradi huu inakuja baada ya kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya Mradi uliotekelzwa katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2016, Awamu hii inayoanzia mwaka 2017 hadi 2021, inakusudia kuwajengea uwezo Wabunge, Watumishi na Wananchi kwa ujumla katika masuala ya utungaji wa sheria, usimamizi wa bajeti ya Serikali pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika Shughuli za Kibunge.

Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza linalojulikana kama *Department for International Delevelopment* – DFID, Serikali ya Sweden, Serikali ya Denmark, Serilkali Ireland na UNDP.

Imetolewana:

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano
Ofisi ya Bunge
DODOMA

13 Septemba,2017.